



KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI

TAARIFA KWA UMMA



Alfajiri ya leo hii tarehe 19 Mei 2024 majira ya saa 11:05, tumepeata taarifa kuwa meli ya MV. Clarias inayofanya safari zake kutoka Mwalo wa Kirumba kwenda Kisiwa cha Godziba Mkoani Kagera imelalia upande mmoja (upande wa kushoto ziwani) wakati imeegeshwa kwenye gati la Bandari ya Mwanza Kaskazini. Meli hiyo ilikuwa imetoka katika safari zake za kawaida zinazofanyika kila siku ya Jumatatu na Ijumaa.

Hadi alfajiri ya leo saa tisa meli hiyo ilikuwa salama lakini kati ya saa 10 na saa 11 alfajiri palisikika mvutano wa kamba (tension) na kisha meli hiyo kulala upande wa kushoto (ziwani).

Meli hii haikuwa na abiria wala mizigo na hivyo hakuna mtu au mali zilizoathirika. Hivi sasa timu ya wataalamu imekutana na inaendelea na jitihada za kuisimamisha meli katika hali yake ya kawaida na kisha timu hiyo itaendelea kufanya uchunguzi ili kubaini chanzo cha tatizo hilo.

Naomba kuuhakikishia umma kuwa vyombo vyetu ni salama na shughuli za uendeshaji kwa meli nyingine za Kampuni ya Huduma za Meli zinaendelea kama kawaida.

Imetolewa na:

Kitengo cha Masoko na Uhusiano kwa Umma.

Mwanza, 19 Mei 2024